



**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**  
**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**  
**WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA**



**MASHARTI YA USAFIRISHAJI VINYAGO NJE YA NCHI**

Msafirishaji wa vinyago nje ya nchi kwa ajili ya zawadi au biashara atatakiwa kufuata taratibu za serikali ikiwa ni pamoja na kukaguliwa, kulipa tozo stahiki na kupatiwa cheti cha kusafirishia vinyago nje ya nchi ( Export certificate) kuendana na Tangazo la Serikali kwa kipindi husika.

**Utaratibu wa kusafirisha vinyago nje ya nchi**

Kabla msafirishaji hajasafirisha vinyago nje ya nchi atatakiwa:-

1. Kufika ofisi za Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania zilizoko katika kila kanda kwa ajili ya ukaguzi wa mzigo wake na kupatiwa Ankara kwa malipo yanayohitajika.
2. Kwa kanda ya Mashariki malipo yanafanyika Makao Makuu ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania zilizoko Mpingo House, Barabara ya Nyerere na Uwanja wa ndege wa Mwalimu Julius Nyerere Dar es Salaam na Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro.

Malipo yote hufanyika benki na kuwasilisha hati ya malipo ofisi za Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania na kupatiwa risiti ya malipo iliyoambatishwa na cheti cha kusafirishia vinyago kitolewacho na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania kabla ya kusafiri.

**Tozo na malipo yanayohitajika:-**

Kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 324 la Tarehe 14, Augusti,2015 limefafanua malipo kwa ajili ya kusafirisha vinyago nje ya nchi kama ifuatavyo:-

Aina ya hati	Thamani ya mzigo	Malipo yanayohitajika (TZS)		
		Fomu ya maombi	Hati ya ukaguzi	Mrahaba (ikiwa mteja amenunua kwa mtu ambaye hajasajiliwa na Wakala)
Ukaguzi	chini ya 300 USD ( Zawadi)	5,000/=	34,500/=	4,600/= kwa kilo kinyago cha mti wa mpingo
	Zaidi ya USD 300	5,000/=	150,000/=	3,000/= kwa kilo kwa

				kinyago cha Miti mingine
Kibali cha kusafirisha/ Cheti	Chini ya USD 300	5,000/=	44,200/= kwa mzigo	
	Zaidi ya 300 USD (mfanya biashara)	5,000	147,200 kwa mzigo	

Msafirishaji wa mzigo wenye thamani kuanzia dola 300 na zaidi anayesafirisha zaidi ya mara moja kwa mwaka atatakiwa kujulikana kama mfanya biashara na atatakiwa kulipa tozo zote kama mfanya biashara na kuwa na nyaraka halali zifuatazo:-

1. Usajili wa kutengeneza au kuchonga vinyago toka Wakala wa Huduma za Misituni.
2. Leseni ya Uvunaji
3. Hati ya kusafirisha mazao ya misitu ndani ya nchi (Transit Pass-TP)
4. Risiti halali ya duka la vinyago linalotambulikana na Wakala wa huduma za Misitu Tanzania.
5. Usajili wa kusafirisha mzigo nje ya nchi

Msafirishaji anayesafirisha mzigo wenye thamani chini ya dola 300 atatambulika kama anasafirisha zawadi na atatakiwa kulipa tozo zote za kusafirishia kama zawadi na atatakiwa kuwa na :-

1. Risiti halali ya kununulia mzigo
2. Nakala ya usajili wa mfanya biashara aliyemuuzia mzigo inayotolewa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania.

Msafirishaji wa zawadi kama mnunuzi ambaye hatakuwa na vitu tajwa hapo juu atatakiwa kulipa mrahaba kulingana na Tangazo la Serikali.

Imetolewa na  
Mtendaji Mkuu  
Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania  
S.L.B 40832 Dar Es salaam, Tanzania  
Simu: +255 22 286 4249; Nukushi +255 22 286 4257; Barua pepe: [mpingo@tfs.go.tz](mailto:mpingo@tfs.go.tz).  
Website: [www.tfs.go.tz](http://www.tfs.go.tz)